# SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA, MAMLAKA ZA WILAYA

**(SURA YA 287 YA 2002)**

---

# SHERIA NDOGO

---

***Zimetungwa chini ya Kifungu cha 160***

---

## SHERIA NDOGO ZA MAMLAKA YA MJI MDOGO BAGAMOYO

## USAFI WA MAZINGIRA 2014

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Mamlaka ya Mji Mdogo Bagamoyo za **(Usafi wa Mazingira)** za mwaka **2014** na zitaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani. jina na **mwanzo wa kutumika**

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo Bagamoyo **Matumizi**

3. Katika Sheria ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:- **Tafsiri**

" **Sheria"** maana yake ni sheria za Serikali za mitaa (Mamlaka ya Wilaya) Sura ya 287 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002

**"Afisa Mtendaji"** ina maana ya **Afisa Mtendaji Mkuu** wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo ikiwa ni pamoja na Afisa ye yote aliyeteuliwa kwa wakati huo kukaimu nafasi ya Afisa Mtendaji Mkuu.

**"Mamlaka"** maana yake ni Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo.

**"Afisa aliyeruhusiwa/Mhidhinishwa,,** ina maana ya mtumishi wa Mamlaka aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

**"Mazingira"** maana yake ni maeneo ya makazi, mtaa, mahali pa starehe na burudani, mtaa/kitongoji nyumba ya kuishi, maeneo ya biashara, ofisi za taasisi, nyumba za kuuzia vyakula, nyumba za makazi ya kawaida;

**"Mazingira machafu"** maana yake ni mazingira ambayo:-

(a) Yana takataka au yakibaki katika hali ya uchafu yanaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa au kuathiri afya za watu au wakazi au yatakuwa

kero kwa wakazi.

(b) Yana harufu mbaya ya mkojo au kinyesi kinachotokana na watu au wakazi wa eneo hilo kulitumia eneo hilo kama sehemu ya kujisaidia.

(c) Yana mitaro au mifereji inayotumiwa na wakazi kama shimo la takataka au ina maji yaliyotuama mahali hapo.

(d) Yana mzoga, mabaki ya vyakula na takataka ngumu za za mifuko ya Plastiki.

(e) Hayana choo, bafu na yana pori au kichaka cha nyasi au miti ambacho hakikutunzwa kwa madhumuni ya mapambo au utunzaji wa mazingira kuzunguka nyumba.

**"Mahali pa starehe"** maana yake ni mahali popote pale ambapo:-

(a) Watu au kikundi cha watu wanaweza kukaa na kutumia eneo hilo kwa ajili ya starehe na burudani.

(b) Panauziwa vinywaji aina yo yote pamoja na baa, stoo, maghala ya vinywaji vikali na baridi.

(c) Nyumba za kulala wageni.

(d) Kumbi za starehe.

**"Mdudu"** maana yake ni mdudu ye yote ambaye anaweza kuharibu vyakula, bidhaa,Vinywaji au kuathiiri mazingira kiasi cha kusababisha magonjwa au kudhuru afya ya binadamu au jamii kwa ujumla na ni pamoja na mbu na inzi.

**"Mkazi"** maana yake ni Mtu yeyote ambaye anaishi ndani ya eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo pamoja na taasisi za Serikali na zileambazo si za serikali ambazo ni mmiliki au mtumiaji wa mazingira.

**"Afisa Mtendaji"** maana yake ni Afisa Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji.

**"Mmiliki"** maana yake ni mtu ye yote ambaye anamiliki ardhi, mahali pa starehe, nyumba za kuuza vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo la makazi yo yote katika mtaa, endapo mazingira husika ni mtaa au barabara za mitaa.

**"Mtaa"** maana yake ni makazi ya watu katika mtaa wote, barabara za mitaa, barabara kuu, uchochoro ulio kati ya nyuumba na nyumba/eneo la wazi katika mtaa pamoja na eneo lililo wazi katika ya sehemu za biashara au mahali pa starehe

**"Mti"** maana yake ni mti wa kivuli, mti wa matunda, mti kwa ajili ya mbao.

**"Nyumba ya chakula"** maana yake ni mgahawa, mama lishe/magenge ya chakula na hoteli na nyumba zote zinazohusika na kuuza vyakula vya aina yo yote.

**"Pipa la takataka"** maana yake ni chombo cha plastiki, bati ama chuma kitakachotumiwa na mkazi au kikundi cha wakazi katika mtaa au eneo fulani ndani ya Mamlaka ya Mji Mdogo kwa ajili ya kutunzia taka ngumu

**"Takataka"** maana yake ni maji machafu, takataka ngumu na laini pamoja na kitu au vitu vilivyotupwa ovyo au kurundikwa katika mazingira ambapo vitu au takataka hizo zinaleta kero kwa watu au endapo hazitachomwa na kuondolewa zinaweza kuleta mlipuko wa magonjwa au mkusanyiko wa wadudu hatari kwa afya, maisha na uhai wa binadamu.

**"Ugonjwa" au "Mlipuko wa ugonjwa"** maana yake ni maradhi au mlipuko wa maradhi ya aina yo yote ile ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu au jamii kwa ujumla, unaweza kujitokeza katika eneo lolote na kwa wakati wowote.

**"Vinywaji"** maana yake ni pamoja na aina yo yote, maziwa, maji ya matunda, maji ya kawaida, soda au kumiminika chochote kinachotumika kama kinywaji.

**"Wanyama" au Mifugo"** ina maana ya wanyama wote wafugwao kama vile ng'ombe mbuzi, kondoo, nguruwe, mbwa, paka na punda na jamii ya ndege

**Wajibu wa mmliki kuweka Mazingira katika hali ya usafi.**

4. Mkazi au Mmiliki atakuwa na wajibu na jukumu la
   (a) kusafisha mazingira yake
   (b) kupanda maua, miti ya kivuli, ya bustani ya mboga na kutunza wakati wote kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Muidhiniwa
   (c) Kuwa na choo na bafu kulingana na matumzi ya idadi ya watumiaji katika kaya/familia
   (d) Awe na pipa la kutupia takataka pembeni ya nyumba yake.
   (e) Kuwa na karo na chanja ya kuanikia vyombo.
   (f) Kuvuta maji machafu katika shimo, karo au vyoo vinapojaa kwa kuzingatia maelekezo ya ushauri wa Afisa Muidhiniwa.ff
   (g) Kutomzuia Afisa Muidhiniwa kufanya ukaguzi
   (h) Kulipia taka anazozalisha
   (i ) Kutotirisha maji machafu.
   (j ) Kusababisha mifereji ya maji ya mvua,na maeneo yote yaliopo mbele ya nyumba

**Marufuku kukata miti kuchoma**

5. Isipokuwa kwa kibali cha maandishi kutoka kwa Afisa Muidhiniwa au kwa madhumuni yaliyokubaliwa na Mamlaka ni Marufuku kwa mtu yeyote yule:-

**moto na kuchunga mifugo Kwenye maeneo ya makazi**

(a) Kukata au kuangusha miti iliyopandwa au kusababisha kung'olewa kwa mboga na matunda ambayo vinatunzwa chini ya sheria ndogo hizi.

(b) Kuchungia mifugo au kusababisha mifugo kuzurura katika bustani za mboga au za miti ya matunda na vivuli ambazo ziko katika nyumba za makazi au mazingira ya aina yoyote ile.

(c) Kusambaza, kutapakaza kinyesi au kujisaidia ovyo haja ndogo katika eneo la makazi au kuchoma moto maeneo au kuweka samadi au kinyesi cha mifugo yake katika mtaa ama barabarani

6. Endapo Mamlaka itaona au kupokea taarifa kwa maandishi/kwa maneno kutoka kwa mkazi ye yote au Afisa Muidhiniwa kuwa kuna bughudha au kero kutokana na kuwepo kwa takataka au uwezekano wa kulipuka kwa magonjwa ya hatari kutokana na kuwepo kwa takataka majumbani au zinazotokana na shughuli za biashara au bidhaa viwandani katika mazingira ye yote yale Mamlaka inaweza:-

(a) Kumchukulia hatua za kisheria mmliki pamoja na kumwamuru kuondoa takataka katika mazingira hayo kwa gharama

(b) Kutoa ilani ya maandishi kwa mmiliki wa eneo hilo kumtaka aziondoe katika mazingira hayo katika muda uliotajwa katika ilani hiyo kwa gharama zake.

(c) Kumweleza Mwenyekiti wa Kitongoji/Mtaa kuwashirikisha wananchi wa eneo husika kuchangia gharama.

(d) Kumwamuru Mwenyekiti wa Kitongoji/Mtaa kusimamia shughuli za usafi wa mazingira pamoja uzoaji wa takataka zilizozagaa hovyo katika eneo lake

7. (1) Ni marufuku kwa mtu ye yote yule kutupa, kurundika, kusababisha Kurundika, au kutupwa ovyo kwa takataka Kwenye mitaa, barabara, au mazingira yo yote.

(2) Ni marufuku kwa mtu ye yote yule kutupa au kusababisha mlundikano wa kifusi cha takataka au udongo, uchafu, mzoga, masalia ya chakula, kutiririsha maji machafu, maji ya vyooni au bafuni katika barabara, mtaa au mazingira yo yote.

(3) Kukojoa na kunya kwenye maeneo ya wazi na makazi.

(4)Kwa yeyote atakayefanya makosa tajwa hapo juu atatozwa faini ya papo Kwa hapo ya shilingi 50,000/= (Hamsini Elfu)

(5)Yeyote atakayembaini mtu atakayetupa taka eneo lilisiloruhusiwa na kuitarifu Mamlaka na hatimaye mhalifu kutozwa faini tajwa hapo juu yule aliyemkamata atalipwa 20% ya faini hiyo.

8. Ni wajibu wa mmiliki wa magari ya abiria kuweka chombo cha kuhifadhi takataka ndani ya gari lake. **Vyombo vya usafiri**

9. (1) Afisa Muidhiniwa atakuwa na wajibu wa:- **Wajibu wa Afisa Muidhiniwa**
   (a) Kukagua usafi kwenye nyumba za makazi.
   (b) Kukagua nyumba za kulala wageni, maduka, na mahali pa starehe na maeneo yote yanayousika.
   (c) Kutoa taarifa ya kila mwezi kwa Afisa Mtendaji kuhusu hali ya Usafi wa mazingira na hatua alizochukua
   (d) Kuhudhuria na kutoa elimu ya Afya kwa wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo Bagamoyo.

(2) Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa:- **Uwezo wa Afisa Muidhinishwa**
   (a) Kuingia na kukagua mazingira yo yote muda wowote atakapoona inafaa.
   (b) Kutoa taarifa (notisi) ya maandishi kwa mhusika akimtaka asafishe Mazingira yake, kwa muda maalum.
   (c) Kuamuru kufungwa kwa shughuli zozote katika mazingira hayo au Kumchukulia hatua za kisheria mmiliki ye yote ambaye hakutekeleza Maagizo yaliyo tolewa katika taarifa au notisi mpaka hapo mmiliki atakapotekeleza.
   (d) Kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mkazi ambaye anashindwa kuweka mazingira ya makazi katika hali ya usafi

(3) Notisi ya taarifa itakayotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya 9 (2) hapo juu itaeleza:-
   (i) Muda wa kutekeleza maagizo au maelezo au ushauri wa Afisa Muidhiniwa.
   (ii) Athari za kutotekelezwa kwa notisi hiyo na mmiliki.
   (iii) Itasainiwa na kupigwa muhuri wa Afisa Muidhiniwa au Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo.

10 - (1) Kutakuwa na ada ya ukusanyaji taka itakayowekwa na kutozwa na Mamlaka ya Mji Mdogo kwenye maeneo yaliyo chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo kwa kuzingatia viwango vilivyoorodheshwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi. **Ada ya ukusanyaji taka**

(2) Ada iliyowekwa na Sheria Ndogo hizi italipwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo au Wakala kabla ya kuzoa taka kwenye eneo husika.

(3) Ukaguzi wa mazingira utafanywa wakati wowote pale afisa mhidhishwa atakapoona inafaa isipokuwa ukaguzi wa dharura unaweza kufanywa pale itakapoonekana ni muhimu kufanya hivyo.

11 – (1) Mamlaka inaweza kumteua mtu binafsi, Kampuni, Taasisi au **Uteuzi**

Shirika kutoa huduma ya kukusanya na kuzoa takataka kwa niaba yake. **wa wakala**

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo ya 11 (1) atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kukusanya takataka kwa kiwango kilichoidhinishwa na Mamlaka

(b) Kuwafikisha Mahakamani wale wote watakaoshindwa au kukataa Kulipa ada ya ukusanyaji taka.

(c) Kuhakikisha kwamba takataka zinakusanywa na kutupwa katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

(d) Kuwasilisha kwenye ofisi za Mamlaka ya mji mdogo ada ya ukusanyaji taka aliyokusanya katika muda uliopangwa.

(e) Kuwasilisha kwenye ofisi za Mamlaka ya mji taarifa sahihi za hesabu walizokusanya.

(3) Wakala yeyote atakayeshindwa kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika sheria ndogo hii, atatozwa (asilimia) 50% ya gharama za makusanyo. **Makosa ya Wakala**

12. Kila muuzaji wa chakula katika nyumba ya chakula atakuwa na wajibu na jukumu na kuhakikisha kwamba **Wajibu wa wauza chakula**

(a) Lazima awe amekaguliwa na amepata kibali cha mamalaka

(b) Chakula kinatunzwa katika hali ya usafi wakati wote.

(c) Chakula kinachouzwa hakijapoa.

(d) Vyombo vya kuuzia chakula, kunywea vinywaji vinatunzwa katika hali ya usafi.

(e) Vyombo vinasafishwa kwa maji ya moto na kupanguswa na kufunikwa kwa kitambaa safi au kuwekwa kwenye kabati lenye kioo kiangavu.

(f) Mazingira ya biashara yake ni masafi wakati wote.

(g)Kuta, sakafu za nyumba, jiko, meza na viti vinasafishwa na kufunikwa wakati wote.

(h) Wafanyakazi katika nyumba yake ya chakula:-

(i) Wamepimwa na kuthibitishwa afya zao na mganga wa serikari

(ii) Wanavaa sare maalum wakati wa kazi na sare hizo ni safi wakati wote

(i) Amelipa ada zote za usafi na ukaguzi wa mazingira kwa muda.

(j) Ana choo, pipa la takataka lenye mfuniko na karo katika mazingira yake na vinakuwa safi wakati wote.

(k)Atahifadhi matunda katika hali ya usafi.

(l)Ataweka chakula mbali na madawa yanayoweza kuhatarisha afya ya binadamu.

(m)Vyakula vyote vilivyopikwa vinahifadhiwa katika vyombo visivyo ingiza vumbi au kuruhusu wadudu kuingia.

13. Katika kutekeleza sheria ndogo hizi, maelekezo yoyote ya Mamlaka ya mji yatatangazwa kwa njia ambayo yatawafikia watu wote ambao yanawahusu au yanaweza kuwahusu. **Maelezo Mamlaka**

14. (1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote:-

(a) Kumzuia au kujaribu kumzuia Afisa muidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya sheria ndogo hizi.

(b) Kumshawishi mtu mwingine kumzuia afisa muidhiniwa asitekeleze wajibu wake au kuzuia shughuli yoyote chini ya sheria ndogo hizi.

(c) Kuongeza jengo, au majengo katika eneo la uwanja ulioidhinishwa na Kujengwa tayari kwa makazi au biashara, bila kibali au taarifa inayoambatana na ramani ya jengo na ukaguzi.

(d) Kuendesha au kufanyia biashara ya pombe ya aina yo yote ndani ya nyumba za makazi.

(e) Kupangisha nyumba kabla haijakaguliwa na kuidhinishwa na Afisa Muidhiniwa kwa makusudi yaliyoandaliwa.

(f) Kuachia maji machafu ya chooni, bafuni au karo kutiririka ovyo barabarani au katika eneo la nyumba yoyote ile.

(g) Kuosha magari, kufulia nguo, kunywesha mifugo na kuoga karibu na kisima cha maji.

(h) Kuuza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo mengine isipokuwa:-

(i) Vyakula hivyo viwe vimetunzwa ndani ya kabati yenye vioo viangavu.

(ii) Vyakula hivyo vinauzwa katika maeneo yaliyotengwa na kuidhinishwa na Mamlaka kuwa ni maeneo ya wachuuzi wadogo wadogo wa vyakula.

(j) Kufanya shughuli za uoshaji wa magari katika eneo lisilohidhinishwa na mamalaka.

(k)Kutotunza maeneo ya kuzunguka nyumba anyokaa/Kiwanja, chake n na kuchafua mifereji ya maji ya mvua

14. (2) Mtu yeyote atakayevunja sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa Na iwapo atakuwa amepatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/= ) au kufungwa jela kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

# JEDWALI

| Na. | Aina ya biashara | Ada ya kuzoa taka taka kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1 | Kaya | 2,000 |
| 2 | Nyumba ya wageni chumba 1-10 | 6,000 |
| 3 | Nyumba ya wageni vyumba 10+ | 10,000 |
| 4 | Mama lishe | 2,000 |
| 5 | Mgahawa | 10,000 |
| 6 | Grocery | 5,000 |
| 7 | Baa | 10,000/= |
| 8 | Mashine ya kusaga | 7,000/= |
| 9 | Mashine ya kukoboa mpunga (watailipa Mamlaka 10,000/= na kusomba wenyewe) | 10,000/= |
| 10 | Mashine ya kupasua mbao(watailipa mamlaka 10,000/= na kusomba wenyewe | 10,000/= |
| 11 | Ofisi za watu na mashirika binafsi | 3,000/= |
| 12 | Hotel ngazi za kitalii (zitabeba zenyewe mpaka dampo, zitalipia ushuru wa dampo) | 80,000/= |
| 13 | Gereji za pikipiki /Bajaji | 10,000/= |
| 14 | Vizimba/vimeza maeneo ya soko | 3,000/= |
| 15 | Maduka madogo ya vyakula | 3,000/= |
| 16 | Maduka ya jumla ya vyakula | 6,000/= |
| 17 | Vibanda vya matunda/mboga | 3,000/= |
| 18 | Vibanda vya chips/Nyama choma | 5,000/= |
| 19 | Maduka ya madawa baridi (Muhimu) | 5,000/= |
| 20 | Saloon za kike na kiume | 5,000/= |
| 21 | Maduka madogo ya bidhaa nyingine | 5,000/= |
| 22 | Maduka ya jumla ya bidhaa nyingine | 5,000/= |
| 23 | Shule za awali kutwa | 15,000/= |
| 24 | Shule za awali kulala | 30,000/= |
| 25 | Shule za Msingi kutwa | 15,000/= |
| 26 | Shule za Msiingi kulala | 30,000/= |
| 27 | Shule za Sekondari kutwa | 15,000/= |
| 28 | Shule za Sekondari kulala | 30,000/= |
| 29 | Vyuo vya Elimu kutwa (chini ya watu 50) | 30,000/= |
| 30 | Vyuo vya Elimu kutwa zaidi ya watu 50) | 50,000/= |
| 31 | Vyuo vya Elimu kulala | 100,000/= |
| 32 | Zahanati | 10,000/= |
| 33 | Vituo vya afya | 20,000/= |
| 34 | Hospitali | 60,000/= |
| 35 | Parking na show-hall za magari/Pikipiki | 12,000/= |
| 36 | Vituo vya mafuta | 15,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 37 | Vibanda vya simu | 1,000/= |
| 38 | Mambo ya kale | 20,000/= |
| 39 | Ofisi za Waongoza Watalii | 6,000/= |
| 40 | Vituo vya kulelea watoto Yatima | 00 |
| 41 | Vilabu vya pombe za kienyeji | 3,000/= |
| 42 | Mabanda ya kuku | 5,000/= |
| 43 | Mamlaka ya Bandari | I00,000/= |
| 44 | Karakana ya useremala | 5,000/= |
| 45 | Stoo za Mkaa | 3,500/= |
| 46 | Wauzaji wadogo wa mkaa | 1,500/= |
| 47 | Kumbi za starehe na Cinema hall. | 4,500/= |
| 48 | Vimeza vya samaki eneo la samaki | 3,000/= |
| 49 | Wachonga vinyago | 1,500/= |
| 50 | Vibanda vya ushonaji | 3,000/= |
| 51 | Malingo ya Miti(vitalo) | 3,000/= |
| 52 | Wasukuma mikokoteni, (Madafu, Matunda na vyakula vingine | 1,500/= |
| 53 | Bucha | 5,000/= |
| 54 | TANESCO | 20,000/= |
| 55 | DAWASCO | 20,000/= |
| 56 | Shirika la Posta | 20,000/= |
| w 57 | Shirika la Simu | 20,000/= |
| a 58 | TRA | 20,000/= |
| 59 | Benki | 20,000/= |
| M 60 | Maeneo ya kukodisha Baiskeli | 1,000/= |
| a 61 | Machinji ya kuku | 5,000/= |
| m 62 | Vituo vya kufyatulia matofali | 5000/= |
| l 63 | Kumwaga maji machafu dampo | 50,000/= |
| a k 64 | Housing estate (watabeba wenyewe mpaka dampo, zitalipia ushuru wa dampo) | 50,000/= |
| a 65 | Kaole Mamba rach | 10,000/= |
| 66 | Viwanda (watabeba wenyewe mpaka dampo, zitalipia ushuru wa dampo) | 100,000/= |
| 67 | Karakana za vyuma | 20,000/= |
| 68 | Vibanda vya kuonyesha video | 10,000/= |
| 69 | Sehemu za kuuzia miti /kuni/mbafo | 15,000/= |
| 70 | Waosha magari (Car Wash) | 15,000/= |

Muhuri wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo ulibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Mamlaka iliyokutana na kuketi tarehe ……………… mwezi ………. 2014 mbele ya:-

……………………

**ATHUMANI O. STILI**
**AFISA MTENDAJI MKUU MJI**
**MAMLAKA YA MJI MDOGO**
**BAGAMOYO**

…………………………..

**ABDUL R. ZAHORO**
**MWENYEKITI**
**MAMLAKA YA MJI MDOGO**
**BAGAMOYO.**

**NAKUBALI**,

………………………

**MWANTUMU BAKARI MAHIZA**
**MKUU WA MKOA**
**PWANI**

**Tarehe**……………………………